NESA NATIONAL EXAMINATION AND SCHOOL INSPECTION AUTHORITY

| Kiswahili |
|---|
| 027 |
| Tarehe: 09/Julai/2025 |
| Wakati: 8.30 AM-11.30 AM |

Majina: ……………………………………

Nambari ya usajili: ……………………………………

**SOMO: KISWAHILI**

**KIDATO CHA SITA**

**MICHEPUO:**
Literature in English-French-Kinyarwanda-Kiswahili **(LFK)**

**MUDA: Masaa matatu (3h00)**

# S6 DAFTARI LA MASWALI NA MAJIBU

**MTIHANI WA TAIFA 2024-2025**

## Maelekezo

1) Usifungue karatasi hii ya mtihani bila ruhusa.
2) Andika majina yako na nambari yako ya usajili kwenye karatasi ya majibu kama vilivyo kwenye fomu yako ya usajili.
3) Mtihani huu una **maswali 22**
4) Mtihani huu umeundwa na sehemu kuu nne:
   - **Sehemu ya I: Ufahamu na msamiati:** Jibu maswali yote **(alama 30)**
   - **Sehemu ya II : Sarufi na matumizi ya lugha:** Jibu maswali yote **(alama 30)**
   - **Sehemu ya III : Fasihi:** Jibu maswali yote **(alama 25)**
   - **Sehemu ya IV : Utungaji:** Chagua mada moja. **(alama 15)**
5) Mwandiko wako usomeke vizuri.
6) Tumia kalamu ya **bluu** au **nyeusi**.
7) **Tahadhari!**: Kwenye maswali ya kuchagua, weka mduara (○) kwenye herufi ya jibu lililo bora.

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| Maswali | Alama | Maswali | Alama |
|---|---|---|---|
| 1 | | 16 | |
| 2 | | 17 | |
| 3 | | 18 | |
| 4 | | 19 | |
| 5 | | 20 | |
| 6 | | 21 | |
| 7 | | 22 | |
| 8 | | 23 | |
| 9 | | 24 | |
| 10 | | 25 | |
| 11 | | 26 | |
| 12 | | 27 | |
| 13 | | 28 | |
| 14 | | 29 | |
| 15 | | 30 | |

**ALAMA: ……………./100**

## SEHEMU YA I: UFAHAMU NA MSAMIATI: (Alama 30)

**Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha ujibu maswali yanayohusika**

***Jongoo na chura***

Hapo zamani palitokea Jongoo na Chura ambao walikuwa marafiki wakubwa sana. Kila wakati walikuwa wanatembeleana.
Siku moja, Chura alimwuliza Jongoo, "Rafiki yangu huwa unafanya nini na ngozi yako? Mbona inang'ara sana! Tazama ngozi yangu, siyo laini. Ningependa iwe kama yako. Hebu nidokezee kidogo".

Jongoo alifurahi kuambiwa kwamba alikuwa na ngozi nyororo. Alianza kumpa rafiki yake ushauri kama ifuatavyo, "rafiki yangu Chura, ngozi hii nyororo unayoiona ni kazi kubwa tena ngumu ambayo mke wangu amekuwa akifanya kwa muda wa miaka mingi. Kila asubuhi huweka kikaango kwenye moto kisha hujaza mafuta...". Kabla hajaendelea na kumaliza, Chura alimkata kauli rafiki yake kwa kusema, "Basi! Basi! Nimeisha elewa. Huna haja ya kunielezea zaidi. Yote haya nitayatenda na utaona nitakavyonawiri".

Jongoo alijaribu kumshawishi amsikilize lakini Chura alisisitiza kwamba kwa utangulizi ule amekwisha elewa kila kitu. Marafiki wale waliagana. Alipofika nyumbani Chura, alimwita mkewe na kumwambia, "Mke wangu! Leo rafiki yangu Jongoo amenieleza jinsi ya kuifanya ngozi yangu iwe nyororo na ya kung'ara kama yake. Sasa hivi ninataka uweke chungu jikoni. Hakikisha jiko lina moto mkali sana".

Mke alifanya kama alivyoelezwa. Chura aliendelea kutoa maagizo, "Ninataka utie mafuta ya kukaangia mboga mengi sana. Yakiisha chemka unieleze mara moja". Mkewe alitekeleza maagizo ya mara kwa mara na kumpa taarifa kwamba mafuta yalikwisha kuchemka. Chura aliingia jikoni akamwambia mkewe, "sasa nitumbukize katika mafuta maana ninataka niibabue ngozi hii ya juu ili ibaki nyororo iliyopo chini yake". Mkewe alipigwa na bumbuazi na kumjibu, "Mume wangu, mbona unaniambia nifanye kitu cha hatari! Ukitumbukizwa katika mafuta haya utapona? Haiwezekani hata kidogo! Balaa hilo!"

Chura alisisitizia kwa ukali kutumbukizwa katika mafuta. Alisema, "Mimi nilikuwa nikikuambia siku zote kwamba ngozi hii inanitia aibu na leo nimepata njia ya kuiondoa, na wewe unapinga! Ukitaka kukaa nyumbani kwangu sharti utimize ninayokuambia kufanya ama sivyo nitakufukuza!"

Mkewe Chura kusikia hivyo, alimnyanyua mumewe na kumtumbukiza katika kikaango. Chura alilia, "Yooooo! Yooooo! Nigeuze upande mwingine!" Mkewe alipomgeuza tu mlipuko mkubwa ulisikika. Chura alipasuka vipande. Utumbo ulitoka katika kikaango na kuanguka chini. Huu ndio ulikuwa mwisho wa mzee Chura.

Mauti ya kujitakia yalimfikia. Mkewe alipoona yaliyokuwa yametokea, alikimbia mara moja na kuwaita majirani. Majirani walikuja kushuhudia msiba. Mjane aliwaelezea jinsi alivyoshurutishwa kumtumbukiza marehemu katika mafuta. Majirani waliamua kwamba mke hakuwa na hatia bali marehemu Chura alisababisha kifo chake mwenyewe kwa ujinga wake.

Huu ndio mwisho wa hadithi!

**Jibu maswali yafuatayo kuhusu kifungu cha habari kilicho hapa juu.**

**<u>Tanbihi</u>:** Kuhusu maswali ya kuchagua, miongoni mwa majibu yaliyotolewa, chagua na uweke mduara (○) kwenye herufi ya jibu lililo bora.

1) Majina ya wahusika wanaozungumziwa ni: **(alama 3)**
   a) Simba, mke wa simba, chura, na majirani wa familia yake.
   b) Sungura, mke wa chura, jongoo, na majirani wa chura.
   c) Fisi, Sungura, Shura, mke wa Chura, Jongoo, majirani wa familia ya Chura.
   d) Chura, Mke wa Chura, Jongoo, majirani wa familia ya Chura.

2) Ni nini kinachothibitisha kwamba Jongoo na Chura walikuwa marafiki? **(alama 4)**
   a) Jongoo alimwomba Jongoo mwenzake wawe marafiki.
   b) Chura alimwambia Jongoo kwamba anampenda sana.
   c) Walikuwa wanatembeleana kila wakati na kupeana maadili.
   d) Walikuwa wanapenda kuchangia kwa kila kitu.

3) Matarajio ya Chura kuhusu ushauri wa Jongoo yalikuwa yapi? **(alama 4)**
   a) Kuweka mafuta katika kikaango, kuyaweka kwenye moto mpaka yakachemka na kujiweka katika mafuta hayo kwa ajili ya kuwa na ngozi laini kama ya Jongoo.
   b) Kuweka mafuta katika kikaango, kuyaweka kwenye moto na kutia chakula chakula ndani kwa ajili ya kuiva na kukila.
   c) Kuweka kikaango kwenye moto kisha hujaza mafuta. Baada ya mafuta kuchemka, chura atayachanganya na dawa nyinyine na kujipaka kwa ajili ya kuwa na ngozi laini.
   d) Kuchemsha mafuta na kuyameza kwa ajili ya kutokuwa na njaa wala kiu.

4) Ni kwa sababu gani Mkewe Chura alipigwa na bumbuazi? **(alama 4)**
   a) Mke wa chura aliona kwamba maagizo ya Chura yanaweza kuhatarisha maisha ya Chura huyo.
   b) Chura alikuwa na nia kumtisha mke wake.
   c) Mke wa Chura aliona kwamba maagizo ya Chura yanaweza kutajirisha familia yao.
   d) Mke wa Chura alifurahia maagizo ya Chura na kutaka kuyatimiza moja kwa moja.

5) Ni kwa sababu gani Chura alikuwa anataka kuiondoa ngozi yake? **(alama 4)**
   a) Ngozi yake ilikuwa na rangi isiyopendeza.
   b) Ngozi yake ilikuwa inaonekana laini sana.
   c) Chura alikuwa na nia ya kutoa manyoya yaliyo kwenye ngozi yake.
   d) Chura alikuwa anataka kubaki na ngozi nyororo iliyo chini yake.

6) Ilikuwaje mke wa Chura alipomweka Chura katika mfuta? **(alama 4)**

a) Ngozi ya nyuma ya Chura iliungua na kutoeka, Chura akabaki na ngozi nyororo iliyokuwa chini yake.
b) Ngozi ya Chura iliungua, akapasuka vipande, utumbo wake ukaangukia chini na kufa papo hapo.
c) Hakuna mabadiliko yaliyojitokeza kwenye ngozi ya Chura.
d) Chura alimshukuru mke wake kwa kumsaidia kuonekana vizuri akiwa na ngozi laini.

7) Majirani walipokeaje kifo cha Chura? **(alama 4)**

a) Walimcheka sana mke wa Chura kwa kusikia kwamba alikubali kumtia mme wake katika mafuta.
b) Walikasirikia mke wa Chura kwa kukubali kutekeleza maagizo ya Chura.
c) Waliona kwamba Chura ndiye aliyejiletea kifo kwa kumshurutisha mke wake kumweka katika mafuta yaliyochamka.
d) Waliona kwamba mke wa Chua alimsaliti kwa kumweka katika mafuta yaliyochemka.

8) Funzo linalotokana na kifungu cha habari hapa juu ni: **(alama 3)**

a) Wema hauozi.
b) Usiache mbachao kwa msala upitao.
c) Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.
d) Siku za mwizi ni arobaini.

**SEHEMU YA II: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (Alama 30)**

9) Weka sentensi zifuatazo katika hali kanushi: **(alama 6)**

a) Badilisha shati au suruali.
b) Mgeni rasmi amewasili.
c) Ukitaka kuishi vizuri fanya kazi kwa bidii.

10) Taja aina ya tungo zifuatazo: **(alama 6)**

a) Mwanafunzi anasoma kitabu.
b) Watoto wanacheza na kupiga ngoma.
c) Ningejifunza vizuri ningepata alama nzuri.

11) Taja aina ya kila neno lililo katika sentensi zifuatazo: **(alama 4)**

a) Mkurugenzi anahutubia wanafunzi wote.
b) Wote walifika shuleni asubuhi.

12) Andika sentensi zifuatazo katika umoja: **(alama 6)**

a) Wezi waliiba ng’ombe usiku huu.
b) Walitupa mawe katika mito.
c) Mbuzi wanapelekwa zizini.

13) Jaza aya ifuatayo kwa kutumia maneno uliyopewa katika mabano. **(alama 5)**

**(bidhaa, kuwasiliana, ulimwengu, maarifa, uwezo)**

Elimu humsaidia mtu kupata ……………… wa kuandika na kusoma. Haya ndiyo …………………. ya kimsingi sana katika kuelimishwa shuleni. Katika ……………………. wa leo, kila kitu hufanyika kwa kuandika na kusoma kama vile: kusoma taarifa za magazeti, kusoma vitabu, kusoma maelezo ya ………………. zinazouzwa madukani, kuweza ………………………….. na watu, kutumia teknolojia ya kisasa, kuelewa matumizi ya vifaa na vyombo vya nyumbani, kusoma maelezo ya matumizi ya dawa mbalimbali n.k.

14) Ni kwa nini lugha rahisi na ya moja kwa moja inapendekezwa katika mwili wa hotuba? Weka mduara kwenye herufi ya jibu moja lililo bora. **(alama 3)**

a) Kufanya hotuba isieleweke kwa wasikilizaji wenye uelewa wa chini.
b) Kuhakikisha ujumbe unafika kwa hadhira pana na kwa urahisi.
c) Kupunguza muda wa maaandalizi ya hotuba.
d) Kuonyesha maarifa ya mzungumzaji kwa kiwango cha juu.

**SEHEMU YA III: FASIHI (Alama 25)**

15) Chagua kwa kuweka mduara kwenye herufi ya jibu la kweli kuhusiana na fasili ya sanaa. **(alama 3)**

a) Kazi ya ufundi yenye kuwahusisha watu wengi katika majadiliano juu ya kazi hiyo.
b) Kazi ya ustadi na ufundi wowote wa kuibusha mawazo yaliyomo katika akili ya binadamu na kuyaonyesha kwa njia mbalimbali.
c) Kazi yoyote yenye kumpa manufaa mbalimbali mtu anayefanya kazi hiyo.

16) Jaza methali zilizo katika aya ifuatayo ili kisa kiwe na maana. **(alama 6)**

Siku moja mkewe Haruna alichelewa kuamka asubuhi. Haruna alimwamsha na kumwonya asizoee tabia hii mbaya ya kuchelewa. Alisema, "…………………………………………… utamkuta mtoto si wako". Halafu, aliendelea kusema, "Mke wangu, 'ndege aamkaye asubuhi………………………………………………………'. Ukiyakumbuka maneno haya, bila shaka tutafanikiwa kwani ……………………………………………………. asemaye kesho ni mwongo. Hili ni onyo mke wangu".

17) Weka mduara kwenye herufi ya jibu moja lililo bora kuhusu tofauti kati ya mashairi ya mapenzi na mashairi ya majigambo. **(alama 3)**

a) Mashairi ya mapenzi yanahusu urafiki kati ya maadui na majigambo yanahusu watu jasiri.
b) Mashairi ya mapenzi yanahusu urafiki kati ya wapendanao na majigambo yanahusu watu jasiri.
c) Mashairi ya mapenzi yanahusu urafiki kati ya wapendanao na majigambo yanahusu watu wenye woga.

18) Jukwaa katika tamthilia linamaanisha nini? Weka mduara kwenye herufi ya jibu moja bora. **(alama 2)**

a) Mahali ambapo tamthilia inaandikiwa wasomaji na watazamaji.
b) Mahali ambapo tamthilia inaonyeshwa mbele ya watazamaji
c) Hali ya kisiasa katika tamthilia.

19) Tumia mshale kuoanisha nahau au misemo ifuatayo kutoka **sehemu A** na maana zake kutoka **sehemu B**: **(alama 5)**

| **Sehemu A** | **Sehemu B** |
|---|---|
| a) Kupiga mali shoka | 1) Kutokuwa na matumaini tena |
| b) Kumezea mate | 2) Kuwa na maneno makali |
| c) Kukata tamaa | 3) Kupata mateso makali |
| d) Kuwa na ulimi wa upanga | 4) Kugawana mali |
| e) Kuona/kupata cha mtema kuni | 5) Kutamani sana |

20) Jibu wa kuandika "**Ni kweli**" kwa kauli iliyo sahihi na "**Si kweli**" kwa kauli iliyo potofu kuhusu umuhimu wa fasihi. **(alama 3)**

a) Fasihi andishi ya vyombo vya sayansi na teknolojia haina mwelekeo kwa kuendeleza jamii.
b) Fasihi andishi huchangia katika maendeleo ya utamaduni wa nchi kupitia maandishi ambayo huzingatia elimu na utamaduni.
c) Fasihi andishi ni sanaa inayomsaidia binadamu kujiendeleza na kuelimika kuhusu historia ya mtu tangu kale na pia kutabiri kisayansi mambo yatakayoathiri binadamu siku za usoni.

21) Ni maana gani ya mashairi ya uzinduzi? Weka mduara kwenye jibu moja ambalo ni bora. **(alama 3)**

a) Ni mashairi yanayomlaza mtu katika hali ya kupumbazwa au kuwa mtumwa bila kupigania haki zake.
b) Ni mashairi yanayomuamsha mtu atoke katika hali ya kupumbazwa au kuwa mtumwa bila kupigania haki zake.
c) Ni mashairi yanayomuamsha mtu atoke katika hali ya kupumbazwa au kuwa mtumwa na kupigania haki zake.
d) Ni mashairi yanayomuamsha mtu aendelee katika hali ya kupumbazwa au kuwa mtumwa na kupigania haki zake.

**SEHEMU YA IV: UTUNGAJI (Alama 15)**

22) Katika maneno kati ya mia mbili (**200**) na mia mbili na hamsini (**250**), tunga insha kuhusu mada moja kati ya hizi zifuatazo hapa chini: **(alama 15)**

a) Faida ya kuhifadhi mazingira.

b) Umuhimu wa kuwa na nidhamu katika maisha yetu.

**-Mwisho-**